# JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI MAKAME

# MKATABA WA UWEKEZAJI ENEO LA HIFADHI YA WANYAMAPORI MAKAME KATIKA KITALU CHA UWINDAJI IRKIUSHIBOUR MAKAME WMA KWA AJILI YA SHUGHULI ZA UWINDAJI WA KITALII

**UMETENGENEZWA CHINI YA KANUNI YA 55(7) NA 64(8) YA KANUNI ZA MAENEO YA JUMUIYA YA HIFADHI ZA WANYAMAPORI ZA MWAKA 2018**

**KATI YA**

**JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI MAKAME**

**NA**

**SUSET TARANGIRE LIMITED.**


**<u>IMETAYARISHWA NA:</u>**

JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI MAKAME,

S.L.P. 153, KITETO - MANYARA
E-mail:………………

# MKATABA WA UWEKEZAJI KWA AJILI YA SHUGHULI ZA UTALII KATIKA KITALU CHA UWINDAJI IRKIUSHIBOUR ENEO LA HIFADHI YA WANYAMAPORI MAKAME

Mkataba huu umefikiwa leo Tarehe ……. ya Mwezi wa ……… Mwaka 2024.

**BAINA YA JUMUIYA YA**

**HIFADHI YA WANYAMAPORI MAKAME**
Hapa atajulikana kama "Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa"
wa Sanduku la Posta Na. 153 Kiteto, Manyara.

NA

**SUNSET TARANGIRE LIMITED**
Hapa atajulikana kama **'MWEKEZAJI'** wa Sanduku la Posta Na. 2150, Arusha - Tanzania.
Kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria ya Makampuni ya Tanzania na kupewa Usajili **Na.138974146)**

**UTANGULIZI**

A. **AMBAPO** Jamii iliyoizinishwa ni Taasisi iliyoasisiwa kwa mujibu wa Sheria ya The Societies Act, Sura 368 ya Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria ya Uhifadhi ya Wanyamapori, (Sura ya 283 ya Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kama ilivyofanyiwa Marejeo Mwaka 2009) na Kanuni za Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori, 2018.

B. **AMBAPO** Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa (Authorized Association) ina Mamlaka ya kuendesha na kuingia katika Mikataba kwa niaba ya Jamii katika eneo Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Makame iliyoko Wilaya ya Kiteto, Mkoa wa Manyara ikiwa ni kwa mujibu wa Katiba ya Jumuiya hiyo. Aidha, Jumuiya husika ina mamlaka na uwezo wa kukubaliana juu ya matumizi ya ardhi katika eneo la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Makame iliyoko Wilaya ya Kiteto, Mkoa wa Manyara.

C. **AMBAPO** Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa imepewa na Mkurugenzi wa Wanyamapori haki ya utumiaji wa rasilimali Wanyamapori kwa matumizi ya uvunaji na yasiyo ya uvunaji katika eneo zima la Jumuiya kulingana na gawio la Rasilimali ya Wanyamapori (quota) litakayotolewa na Mkurugenzi wa Wanyamapori kwa kipindi husika kwa ajili ya uvunaji endelevu.

D. **AMBAPO** Mwekezaji ameomba kwa Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa kukodisha Kitalu cha uwindaji Irkiushiobor kwa ajili ya shughuli hiyo kwa mujibu wa Mpango wa Jumla wa Usimamizi wa Rasilimali (GMP) kwa lengo la kufanya shughuli za uwindaji wa kitalii.

E. **AMBAPO** Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa na Mwekezaji kwa mujibu wa kifungu cha 31(7) cha Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori Namba 5

ya Mwaka 2009 imeingia katika Mkataba kuwezesha Mwekezaji kufanya shughuli za uwindaji wa kitalii katika Kitalu cha Uwindaji Irkiushiobor kwa ajili ya shughuli hiyo kwa mujibu wa Mpango wa Jumla wa Usimamizi wa Rasilimali (GMP), na kwa pamoja pande zote husika zimekubaliana na vigezo na masharti kama yanavyoonekana katika mkataba huu.

F. **AMBAPO** Kitalu cha Irkiushiobor ambacho kinakusudiwa kwa ajili ya uwekezaji kitaendana na mpaka wa Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Manyara uliotafsiriwa ardhini mnamo mwezi Juni 2023 na hakitavuka mpaka wa Mkoa wa Manyara. Eneo la Kijiji cha Irkiushiobor Wilayani Kiteto Mkoani Manyara analopangishwa Mwekezaji litazingatia mipaka ya Kiutawala iliyopo katika Mkoa wa Manyara kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Namba 367 la mwaka 2002 lililotangaza Mikoa ya Arusha na Manyara.

**KATIKA MKATABA HUU IMEKUBALIKA KAMA IFUATAVYO:**

**1. LENGO LA MKATABA:**

a) Kukusanya pamoja ujuzi, maarifa, fedha na mali (Assets) ya Jamii husika kwa lengo la kuleta maendeleo kwa kutumia rasilimali Wanyamapori na shughuli nyingine za kiuchumi zinazoandamana na rasilimali hizo katika eneo la Jumuiya.

b) Kutoa ujuzi unaohitajika wa kiufundi, kifedha na kiutawala kwa ajili ya mafanikio ya mradi wa uwekezaji.

c) Kuhakikisha kuwa wanajamii wa eneo husika wanapata gawio la haki na manufaa kutokana na utumiaji wa rasilimali zilizopo katika eneo la uwekezaji na pia kuhakikisha kuwa maslahi ya Mwekezaji yanalindwa na kupata kinga ya katika madgubuti katika uwekezaji aliyoufanya.

**2. WAJIBU WA WAHUSIKA**

**2.1 Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa inamuhakishia Mwekezaji kutekeleza Masharti yafuatavyo: -**

a) Jumuiya itampa Mwekezaji au wakala wake haki ya kuingia katika eneo la uwekezaji katika kipindi chote cha uhai wa Mkataba huu pasipo usumbufu wowote.

b) Jumuiya haitatoa haki ya matumizi kwa Mtu au Taasisi/Kampuni nyingine ya kuendesha Biashara ya uwindaji wa kitalii katika eneo la uwekazaji katika kipindi chote cha uhai wa Mkataba huu.

c) Jumuiya itamwarifu Mwekezaji na kumhusisha katika mambo yote ambayo Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa itaamini kuwa yatakuwa na athari katika kuendelea kuwepo kwa uwekezaji husika katika Mkataba huu au shughuli za Mwekezaji katika eneo la Jumuiya.

d) Jumuiya haitaingia katika mkataba mwingine wowote au kuungana na chombo chochote kingine ambacho utekelezaji wake utaleta madhara katika shughuli za Mwekezaji bila ya kumuarifu kabla ya kutaka kufanya hivyo na kupata ridhaa ya Mwekezaji.

e) Jumuiya ina wajibu wa kuitisha mikutano ya kiutawala /menejimenti kila baada ya miezi sita (06) ambapo mwaka mmoja itaitisha vikao viwili kwa lengo la kujadili maendeleo, changamoto na kuazimia shughuli za mwaka unaofuata, Aidha ,Jumuiya itakuwa na wajibu wa kuitisha vikao vya dharura (Extra Ordinary Meetings) na kufanyika katika ratiba kadiri kati ya mwekezaji na jumuiya.

f) Jumuiya itakuwa na wajibu wa kuunda Kikosi Kazi (Joint Task Force) kitakachoratibu utekelezaji wa Mkataba huu kila baada ya miaka mitatu (3) Wajumbe wa kikozi kazi watatokana na wawakilishi kutoka kwenye Jumuiya na maafisa waandamizi kutoka kwa mwekezaji.

g) Jumuiya itakuwa na wajibu wa kuchukua hatua stahiki katika kutunza na kuendeleza eneo lote Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori na kuhakikisha kwamba eneo hili halitumiki kwa shughuli za kilimo na makazi ya kudumu.

**2.2 Mwekezaji anahakikishia Jumuiya kutekeleza Masharti yafuatayo:**

i. Mwekezaji atatoa fedha zilizokubalika kwa mujibu wa mkataba huu ili kutimiza azma ya mkataba huu ikiwemo kuboresha na kuendeleza ufanisi yote ambayo inahitajika kwa ajili ya ufanisi wa biashara iliyowekezwa.

ii. Mwekezaji atatoa vifaa na mali zinazohitajika kutolewa kwa mujibu wa mkataba huu ili kutimiza azma ya mafanikio ya uwekezaji huo.

iii. Mali yote isiyohamishika na mali ya kudumu ambayo kuondolewa kwake kunaweza kuleta madhara kwa mazingira itakuwa mali ya Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa baada ya mkataba huu kufikia ukomo.

iv. Mwekezaji atajenga na kutunza majengo yote muhimu kwa uwekezaji huo na kabla ya kufanya hivyo atatakiwa kupata ridhaa ya maandishi kutoka kwa Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa.

v. Ataheshimu utamaduni na mila za jamii ya eneo hilo na kwamba hataingilia shughuli za kijamii

vi. Hataihusisha Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa katika athari za kifedha za aina yoyote ile au uwajibikaji unaohusiana na mkataba huu.

vii. Atalitangaza eneo la Jumuiya ndani na nje ya nchi.

viii. Atafundisha na kuajiri wakazi wa eneo husika katika shughuli za kila siku za mradi huo. Mwekezaji atatakiwa kuajiri si chini ya asilimia 60 ya wafanyakazi wake kutoka kwa wakazi wa eneo hilo.

ix. Mwekezaji hataingilia, kuvuruga au kutumia nyenzo za kisiasa, kifedha au kiuchumi kwa namna yoyote ile kwa lengo la kushinikiza shughuli za kila siku za utawala za Jumuiya kwa faida yake.

x. Mwekezaji hatatumia ardhi iliyotolewa kwa ajili ya uwekezaji kwa matumizi mengine tofauti na ya yale yaliyokubalika na kuelezwa katika Mkataba huu. Aidha, iwapo Mwekezaji atakuwa na nia ya kutumia ardhi kwa lengo tofauti atawajibika kupata kibali cha maandishi kutoka kwa Jumuiya.

xi. Mwekezaji hatapangisha au kuhamisha utekelezaji wa mashrti ya utekelezaji wa mkataba huu kwa mtu, Taasisi au Kampuni bila ya kupata kibali cha maandishi cha Jumuiya ambacho kitatolewa na mkutano mkuu wa Jumuiya uliohitishwa kihalali kwa madhumuni ya kujadili na kuafikia ombi la kutoa kibali hicho.

xii. Mali yote inayohamishika na isiyohamishika inayotumika katika shughuli za uwekezaji huo itakuwa ni mali ya Mwekezaji katika uhai wa Mkataba huu na kwamba Mwekezaji hataazima, kukodisha au kupangisha mali yoyote isiyohamishika kwa ajili ya kutumia bila ya kupata kibali cha maandishi cha Jumuiya.

xiii. Mwekezaji atashirikiana na jumuiya ya jamii iliyoidhinishwa katika kusimamia rasilimali ya Wanyamapori ndani ya eneo husika katika Mkataba huu kwa lengo la kuwanufaisha wananchi wake.

xiv. Mwekezaji atashiriki katika kutoa wa Elimu ya Uhifadhi kwa jamii inayomzunguka na WMA kwa ujumla wake.

xv. Mwekezaji atachimba visima vitano vyenye Thamani ya Shilingi za Kitanzania **Milioni Mia Mbili** katika vijiji Vitano (05) vya Jumuiya katika kipindi cha Miaka Mitano (05) mara baada ya mkataba kuanza, ambapo kila kisima kitakuwa na Thamani ya Shilingi za Kitanzania **Milioni Arobaini**.

xvi. Mwekezaji atajenga wodi ya wanawake yenye Thamani ya Shilingi za Kitanzania **Milioni Mia** katika mwaka wa tatu wa utekelezaji wa Mkataba huu, wodi husika itajengwa katika kijiji kitakachopendekezwa na jumuiya.

xvii. Mwekezaji atatoa sare Jozi 90 kwa Askari 45 zitakazotolewa mara Mbili katika utekelezaji wa mkataba wake ambapo jozi 45 zitatolewa mwaka wa Nne na jozi 45 zitatolewa Mwaka wa Nane.

**2.3 Masharti ya Shughuli za Uwindaji wa Kitalii**

i. Mwekezaji atatoa huduma za msingi za kijamii kama ilivyokubaliwa katika Mkataba.

ii. Mwekezaji atawaruhusu Wanajamii/Wakazi wa eneo husika ikiwa ni baada ya kupata kibali kutoka kwa Jumuiya, kuingia katika eneo la Jumuiya kwa ajili ya kufanya ibada na matambiko ya kimila iwapo shughuli hizo hazitakuwa na madhara kwa vifaa na shughuli za uwekezaji.

iii. Mwekezaji atatoa Motisha ya Shilingi za Kitanzania Laki Tano (TZS.500,000/=) kwa kila mwananchi au kikundi kitakachotoa habari za siri (*informer*) zitakazofanikisha kuwafichua, kukamatwa na kufikishwa Mahakamani jangili/majangili na vifaa vilivyotumika katika ujangili.

iv. Mwekezaji atatoa Motisha ya Shilingi za Kitanzania Laki Mbili (TZS.200,000/=) kwa mtoa taarifa (Informer) atakayefanikisha kukamatwa Bunduki iliyotumika katika ujangili.

**3. USIMAMIZI WA MALIASILI**

Mwekezaji anakubali kutekeleza yafuatayo: -

a) Kuchukua hatua zote muhimu kuzuia mmomonyoko wa udongo na uharibifu mwingine wa ikolojia ndani ya eneo la Jumuiya.
b) Kutokuondoa, kuuza, kuharibu au kuruhusu kuondolewa kwa mchanga, changarawe, udongo, mawe au mbao katika eneo husika katika Mkataba huu.
c) Kutokata miti yoyote bila kibali cha maandishi cha Jumuiya.

**4. KUGAWA AU KUACHIA UMILIKI**

Mwekezaji anaahidi kwamba hatapangisha, hatakabidhi wala kumpa mtu au kutoa kwa mtu yoyote umiliki wa haki yake au kifaa au nyenzo yoyote au sehemu yake ambayo imetolewa kwa ajili ya uwekezaji na Jumuiya chini ya Mkataba huu.

**5. DHAMANA YA UTEKELEZAJI**

Ili kulinda Haki na Maslahi ya pande zote Mbili, Wahusika katika mkataba huu wanakubaliana kama ifuatavyo;

5.1 Mwekezaji atatoa dhamana kwa ahadi zake zote alizoahidi kutekeleza ndani ya muda wake wa uwekezaji katika Kitalu cha Irkiushiobor.

5.2 Mwekezaji atatakiwa kuwasilisha hati ya dhamana yaani **Security Bond** ya utekelezaji wa mkataba huu yenye thamani ya ya Dola za Marekani 20,000 kutoka katika taasisi za kifedha yaani Bank zinazotambulika kisheria ikiwa ni dhamana ya utekelezaji wa Mkataba huu.

5.3 Dhamana ya Mkataba (**Security Bond**) itakayowasilishwa na Mwekezaji kwa mujibu wa kifungu cha 5.2 itakuwa inapungua na kuhuishwa kila Mwaka kulingana na utekelezaji wa ahadi Mwekezaji atakaokuwa ametekeleza.

**6. ADA KWA AJILI YA HAKI YA KUENDESHA SHUGHULI**

Ada kwa ajili ya haki ya kuendesha biashara ya safari zitatolewa kwa kufuata viwango vifuatavyo:

6.1 Mwekezaji atalipa jumla ya kiasi cha **USD. 150,000.00** kwa mwaka kama ada ya Kitalu cha Uwindaji.

6.2 Kiasi cha ada iliyotajwa katika aya 6.1 inajumuisha **USD 30,000.00** kama ada ya kitalu kwa mujibu wa kanuni na **USD 120,000.00** ikiwa ni nyongeza ya ada ya kitalu.

6.3 Mwekezaji atalipa jumla ya kiasi cha **USD. 15,000.00** kwa mwaka kama michango kwa ajili ya Maendeleo ya Jamii

6.4 Kiasi cha ada iliyotajwa katika aya 6.3 inajumuisha **USD 5,000.00** kama ada ya michango ya maendeleo ya jamii kwa mujibu wa kanuni na **USD 10,000.00** ikiwa ni nyongeza ya michango ya maendeleo ya jamii

6.5 Mwekezaji atalipa jumla ya kiasi cha **USD. 18,000.00** kwa mwaka kama michango kwa ajili ya ulinzi wa wanyamapori

6.6 Kiasi cha ada iliyotajwa katika aya 6.5 inajumuisha **USD 5,000.00** kama ada ya michango ya ulinzi wa wanyamapori kwa mujibu wa kanuni na **USD 10,000.00** ikiwa ni nyongeza ya michango ya ulinzi wa wanyamapori kwa ajili ya doria na **USD 3,000** ikiwa kwa ajili ya chakula cha askari wakati wa doria.

6.7 Kiasi cha **USD 30,000.00** kilichotajwa katika aya ya 6.2 kitalipwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori ambaye atazigawanya kwa mujibu wa mgawanyo wa mapato kama ilivyoainishwa kwenye kanuni za maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori. Aidha kiasi cha **USD 120,000.00 cha nyongeza ya ada, USD 15,000 ya michango ya maendeleo ya jamii na USD 18,000 ya Ulinzi wa Rasilimali** italipwa moja kwa moja kwenye akaunti ya Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa kwa akaunti namba

JINA: MAKAME, HIFADHI YA WANYAMAPORI.
Namba ya akaunti: 50103300149
Tawi la Kibaya Benki ya NMB

6.8 Ada na Tozo zilizotajwa katika aya ya 6.1, 6.3 na 6.5 hapo juu kwa Mwaka **2024** italipwa mara tu baada ya Mkataba huu kusainiwa. Kuanzia Mwaka **2025** na kuendelea ada hii italipwa kabla ya Tarehe 31 Mwezi wa Machi ya Mwaka husika kwa kipindi chote cha utekelezaji wa mkataba huu.

## 7. MATENDO YANAYOZIDI UWEZO WA BINADAMU.

Katika Mkataba huu, hakuna upande utakaohusika kwa kushindwa kutekeleza majukumu yake iwapo kushindwa huko ni kutokana na matokeo ya majanga ya asili kama vile; moto, mafuriko,tetemeko la ardhi na dhoruba, au maafa mengine kama vita, uvamizi wa hifadhi au uvamizi kutoka nchi nyingine, vita ya wenyewe kwa wenyewe, uasi, mapinduzi ya kijeshi au nguvu ya kuondolewa madarakani, shughuli za kigaidi, kutaifisha, Serikali kuidhinisha, kufungana, vikwazo, kazi ya mgogoro, mgomo, mabadiliko ya Sera na Sheria za nchi.

**8. SHERIA ITAKAYOTUMIKA, USULUHISHI NA UTATUZI WA MIGOGORO**

Mambo yote yanayohusiana na Mkataba huu yataongozwa na Sheria na taratibu kwa mujibu wa Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**9. MARIDHIANO/USULUHISHI**:

Endapo patokea kutoelewana, mgogoro wowote ule baina ya pande mbili zilizopo katika Mkataba huu au/na mtu yoyote anaedai haki au kutokuelewa katika jambo lolote linalohusiana na tafsiri ya kifungu chochote au kuvunjwa kwa kifungu chochote au kusitishwa kwa Mkataba huu kwa namna yoyote ile, shauri hilo litatuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Usuluhishi (Arbitation Act, Cap. 15).

Shauri hilo linaweza kusikilizwa kwa pande zote kuwepo mbele ya Mwamuzi/Waamuzi au kwa njia yoyote hata ya kielektoniki kurahisisha usikilizwaji na kwa wakati. Lugha itakayotumika katika shauri hilo ni Kiswahili au Kiingereza kutegemeana na muktadha na mazingira.

**10. UTUNZAJI NA UONAJI WA KUMBUKUMBU**

Mwekezaji atatunza na kuweka kumbukumbu na vitabu vya mahesabu na kuvitoa kwa Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa kwa ajili ya ukaguzi pale vitakapohitajika.

Mwekezaji atatoa vitabu na kumbukumbu hizo kwa ajili ya Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa kujiridhisha juu ya mwenendo wa shughuli ya uwekezaji.

**11. UENDESHAJI NA MUDA**

Mkataba huu ni wa kipindi cha Miaka Kumi (10) tu na ambapo utaanza tarehe 11 Mwezi 05, 2024 na kukoma tarehe 11 Mwezi 05 Mwaka 2034.

**12. MAREKEBISHO.**

Pande zote zinaweza kwa makubaliano kuufanyia marekebisho Mkataba huu au sehemu kifungu chochote iwapo wataona kufanya hivyo ni muhimu ikiwamo kukidhi haja ya mabadiliko ya sheria, kanuni, sera au pale inapoonekana kuwa inafaa kufanya hivyo ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Mkataba. Pamoja na hivyo, wahusika wanakubaliana kuwa kila baada ya Mwaka Mmoja watafanya mapitio ya Mkataba huu kwa kuzingatia mwenendo wa mapato na kufanya maboresho kwa kadiri itakavyofaa. Endapo itabainika kuwa hakuna ongezeko la msingi la mapato makubaliano ya awali ya Mkataba yataendelea.

**13. KUSITISHWA KWA MKATABA**

a. Mkataba huu utasitishwa moja kwa moja ikitokea Mkurugenzi wa Wanyamapori ameondoa au amefuta Kibali au Haki ya Matumizi ya Rasilimali ya Wanyamapori iliyotolewa kwa Jumuiya.

b. Upande wowote wa Mkataba utakuwa na haki ya kusitisha Mkataba huu ikitokea upande mwingine wa Mkataba umefanya uvunjaji mkubwa (*fundamental breach*) wa Mkataba kwa kutoa Notisi ya Siku 90. Uvunjaji Mkubwa wa Mkataba utajumuisha, lakini hautabanwa tu katika yafuatayo:-
   i. Mwekezaji au Jumuiya iliyoidhinishwa kushindwa kutekeleza majukumu au wajibu wowote aliopewa chini ya vifungu vilivyomo katika mkataba huu, na akashindwa kurekebisha uvunjaji huo ndani ya siku 60 baada ya kupewa taarifa (notisi) ya kurekebisha uvunjaji huo kutoka upande mwingine.
   ii. Ikiwa Mwekezaji atafilisika au kampuni itafungwa kisheria isipokuwa kama Mwekezaji atakuwa anaundwa upya kisheria (*reconstruction*) au kuunganishwa.
   iii. Ikiwa Mwekezaji atachelewesha kumalizika kwa uwekezaji pale ambapo walikubaliana muda wa kuanza uwekezaji toka siku ya kusaini Mkataba na ikiwa siku hiyo ilikubaliwa kwa maandishi na wahusika.
   iv. Bila kujali haya yote, Jumuiya Iliyoidhinishwa, inaweza kusitisha Mkataba huu kwa kuangalia manufaa yake.

c. Endapo Mkataba utasitishwa iwapo, Mwekezaji atasimamisha shughuli zake mara moja, na kulifanya eneo la uwekezaji salama na kuondoka ndani ya siku 90.

d. Endapo Mkataba utasitishwa kwa ajili ya kuzingatia manufaa ya Jumuiya iliyoidhinishwa au kutokana na uvunjaji mkubwa wa Mkataba kwa Jumuiya; wahusika wataweka Mthamini Huru (*Independent Valuer*) atakayetoa Hati Maalum ya thamani ya Gharama za Mwekezaji na kisha uthamini wa *Independent Valuer* uidhinishwe na Mthamini Mkuu wa Serikali katika eneo ambalo Mwekezaji atatakiwa kufidiwa.

**14. FIDIA**

Pande zote zinakubaliana hapa kuwa Mkataba huu utakapoisha au kusitishwa basi: -

a) Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa itaweza Mwekezaji kuondoa uwekezaji alioufanya kwa maslahi yake kama taasisi ndani ya eneo la uwekezaji na kumtaka kuirejesha ardhi katika hali inayokubalika kwa Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa katika kipindi cha Miezi Mitatu ya kalenda.

b) Itakapotokea kuwa Mwekezaji ameshindwa kuondoa uwekezaji huo alioufanya basi Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa mara baada ya muda wa notisi ya miezi 3 kuisha wanaweza kuondoa uwekezaji huo kwa lengo la kurejesha ardhi katika hali yake ya awali na kuchukua fedha kwa kazi hiyo kutoka kwenye dhamana

aliyoweka Mwekezaji kama ulinzi wa utekelezaji wa mkataba huu.

c) Iwapo itatokea kwamba Mwekezaji hadai maendeleo yoyote yaliyofanywa naye kwa maslahi ya utendaji wa taasisi yake basi mali yote isiyohamishika itahamia kwa Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa na hakutakuwepo na ulipaji wa fidia yoyote ile.

**15. NOTISI/TAARIFA.**

Notisi au taarifa yoyote au mawasiliano ya kimaandishi yatatumwa au kupelekwa kwa wahusika na kila muhusika atachukuliwa kuwa ametumiwa au amepokea notisi/taarifa ikiwa tu notisi/taarifa hiyo itawasilishwa kwake kwa barua ya rejista na barua pepe.

Mwekezaji ikiwa notisi/taarifa itatumwa kwa;

**SUNSET TARANGIRE LIMITED,**
**S.L.P. 2150, ARUSHA.**
**Barua Pepe: ....................**

Jumuiya ya Jamii Iliyoidhinishwa ikiwa notisi/taarifa itatumwa kwa;

**KATIBU,**
**JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI MAKAME,**
**S.L.P. 153, KITETO, MANYARA.**
**Barua Pepe: manager@makame.org.tz**

**16. GHARAMA.**

Kila upande katika mkataba huu utajigharamia gharama zake halali na masurufu zihusuzo maandalizi na usajili wa Mkataba huu.

**17. HAKUNA UTENGUAJI WA HAKI.**

Kushindwa kutekeleza ama kuchelewa katika utekelezaji wa haki ama nafuu chini ya Kanuni ama Mkataba huu hakumaanishi utenguaji wa haki husika ama nafuu ama kuondosha haki ama nafuu nyinginezo. Hakuna utekelezaji ama sehemu ya utekelezaji wa haki ama nafuu unaoelezewa katika Sheria ama Mkataba huu ama utekelezaji wa haki na nafuu nyinginezo. Haki na nafuu chini ya Mkataba huu ni jumuisho wala hazibagui haki na nafuu zitolewazo na Sheria.

**18. MAKUBALIANO KWA UJUMLA**

a) Mkataba huu na makubaliano yaliyomo ndani yake unawakilisha maelewano ya pande husika na hakuna makubaliano mengine baina ya wahusika kuhusiana na mada ya Mkataba huu, na hakuna mabadiliko ama marekebisho ya Mkataba huu yatakayokuwa na maana ama kuubana upande wowote husika isipokuwa kama;

   i. yamefanywa kwa maandishi,
   ii. yana Hadidu za Rejea kwenye Mkataba huu,

iii. yametiwa saini na wahusika wa Mkataba huu ama wateule wao.

b) Kwa ajili ya uzingatiaji ama utekelezaji, vipengele vyote vya Mkataba huu vitaendelea kuwa na nguvu zote na ushawishi bila ya kujadili kwamba Mkataba umeisha.

**KWA USHUHUDA HUU BASI**, Upande wa Mwekezaji na Upande wa Jumuiya iliyoidhinishwa katika Mkataba huu wanashuhudia Mkataba huu kwa kuweka sahihi zao kwa namna inavoonekana hapa chini;

**MKATABA HUU** umewekwa **SAHIHI** na **KUPIGWA MUHURI** na **JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI MAKAME** na kupokelewa Mbele yetu leo Tarehe ______ Mwezi _________ 2024.

**MUHURI**

JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI MAKAME (JUMUIYA... WMA) INDEMA MAKAME

JINA: LENDUKUSHI KEIYA

SAINI: [signature]

CHEO: MKITI WA BODI YA WADHAMINI

TAREHE: 11/05/2024.

JINA: CPA. HAWA ABDUL HASSAN

SAINI: [signature]

CHEO: MKURUGENZI MTENDAJI (W) KITETO

TAREHE: 11/05/2024

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
KITETO

**Mbele yangu:**

Jina: CHRISTOPHER DONALD

Wadhifa: WAKILI

Sahihi: [signature]

CHRISTOPHER DONALD MWAKIBIBA
Advocate
Notary Public
&
Commissioner
For Oaths
P.O. Box 79341, ILALA-DSM

**MKATABA HUU** umewekwa **SAHIHI** na **KUPIGWA MUHURI WA MOTO** na **SUNSET TARANGIRE LIMITED** na kupokelewa mbele yetu leo tarehe____ Mwezi ____________ 2024. Hapa Arusha – Tanzania.

**MUHURI.**

SUNSET TARANGIRE LIMITED
P.O. Box 15128
ARUSHA

JINA: SALEH Sahim Alamry

SAINI: [signature]

CHEO: MKURUGENZI

TAREHE: 11-5-2024

JINA: Raymond Mdoe

SAINI: [signature]

CHEO: OPP. MANAGER

TAREHE: 11/5/2024

**Mbele yangu:**

Jina: CHRISTOPHER DONALD

Wadhifa: WAKILI

Sahihi: [signature]

CHRISTOPHER DONALD MALWIBA
Advocate,
Notary Public
&
Commissioner
For Oaths
P.O. Box 79341, ILALA-DSM



[signature] [signature]